# GUNDUA KIPAJI CHAKO

MADA YA

1

***Alama ya Chapisho***

Februari 2022

Programu ya ‘Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?’ linaweza kuwa huru kutumika, kwa vile chanzo kimetajwa.

***Ilianzishwa na:*** Wil Bom, VSO, mradi wa Vijana na Ajira, Zanzibar, Tanzania

***Kwa ushirikiano na:*** Walimu na wakufunzi wasaidizi wa makundi manne ya Mafunzo ya Ufundi (Amali), Unguja na Pemba; Sophie Oonk wa Randstad Uholanzi ambaye aliendeleza mada ya 5 ‘Gundua biashara yako’; Kitty den Boogert, rafiki na mwenzangu wa zamani, ambaye aliangalia toleo la mwisho.

***Kwa kuzingatia:*** Warsha (ya mafunzo) ya maendeleo ya kazi, iliyotolewa wakati wa maonesho ya Zanzi Job ya mwaka 2015 na 2016.

Utangulizi wa VSO-ICS juu ya uajiri na ujuzi wa maendeleo ya kazi katika mwaka 2015 na warsha (za mafunzo) zilizotolewa na Watu wenye Kujitolea wa Huduma za Wananchi, Kimataifa.

Mwongozo wa mafunzo, Elimu ya Ujasiriamali na Mafunzo ya EET, Kuboresha Uwezeshaji wa Kiujasiriamali, Moduli ya 1 na 2, VETA, 2014 – 2008.

Maendeleo ya programu kwa mwongozo wa kazi katika mafunzo ya ufundi na CINOP, Uholanzi. www.cinop.nl

Loopbaanmagazijn (Hifadhi ya kazi), ilianzishwa na Claudine Hogenboom, mradi wa Mwongozo wa Kazi kwa mafunzo ya ufundi, Uholanzi. http://www.expertisepuntlob.nl/

Het lespakket netwerken (Mtandao wa Mtaala), ilianzishwa na La Red B.V., Uholanzi. http://lared.nl/

***Tafsiri ya Kiswahili:*** Abdalla Baruan, Dar es Salaam, abbybaruan@gmail.com
Abraham Mtongole, Dodoma, abmtongole@gmail.com
Yahya Abdu, Pemba, Tafsiri ya kiswahili na uhakiki wa toleo la mwisho, yahyarashid@live.com

***Ubunifu:*** Katie Wolgemuth, VSO Dar es Salaam na wanafunzi wa GLU, Grafisch Lyceum Utrecht

***Ilichapishwa na:*** VSO Tanzania, S.L.P 6297, Dar es Salaam Tanzania

***Eneo:*** Ploti na. 997 Msasani, Barabara ya Chole, Dar es Salaam Tanzania

***Simu:*** (+255) 222600072 au (+255) 222600087


***Barua pepe:*** vsotanzania@vsoint.org

***Tovuti:*** www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet




# MAENDELEO YA KAZI NAMNA YA KUWAONGOZA VIJANA KWENYE MAFUNZO YA UFUNDI NA AJIRA AU AJIRA BINAFSI?

## MADA YA 1 GUNDUA KIPAJI CHAKO



# YALIYOMO

Kitabu hiki 'Gundua kipaji chako' ina vifaa kwa ajili ya mada ya 1 ya programu kwenye Maendeleo ya Kazi. Kwanza, unakuta utangulizi wa jumla kwenye programu na namna ya kuandaa mafunzo. Hii inafuatiwa na maelezo mahsusi ya jumla ya mazoezi ya mada ya 1, maelekezo tofauti kwa kila zoezi na karatasi za mazoezi.


Utangulizi wa jumla Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi naa jira au ajira binafsi? 6 - 11

Mada ya 1 na maelezo ya jumla ya mazoezi 'Gundua kipaji chako' 12 - 15

Mada ya 1: mazoezi 1.1 - 1.20 16 - 55

Karatasi za mazoezi 56 - 69


Vichwa vya vitabu vyote sita vya programu ya Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi? ni:

1 Gundua kipaji chako
2 Gundua shauku yako
3 Gundua ulimwengu wako wa kazi
4 Gundua mtandao wako
5 Gundua biashara yako
6 Mpango kazi wako na kuomba kazi

Uwasilishaji wa pawapointi na karatasi za mazoezi zinaweza kupakuliwa kutoka www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet

# UTANGULIZI WA JUMLA

# MAENDELEO YA KAZI: NAMNA YA KUWAONGOZA VIJANA KWENYE MAFUNZO YA UFUNDI NA AJIRA AU AJIRA BINAFSI?

**Mradi wa VNA na programu ya 'Ulimwengu Wangu wa Kazi'**
Vijana na Ajira (VNA), mradi wa Vijana na Ajira ni moja ya miradi ya VSO, Volunteer Services Oversee (Huduma za Kujitolea, Ng'ambo) kwa ushirikiano na RGZ, (Revolutionary Government of Zanzibar/Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar). Moja ya vipengele vya mradi wa VNA ni programu ya 'Ulimwengu Wangu wa Kazi' (UWwK).

Programu ya UWwK hutaka kuimarisha nafasi ya kijamii na kiuchumi ya vijana ndani ya Zanzibar kwa kuendeleza ustadi mbalimbali wanaouhitaji kwa ajili ya ajira, ajira binafsi au ujasiriamali. Kwa kusudio hilo, viunganishi madhubuti zaidi baina ya sekta binafsi na mafunzo ya ufundi ni muhimu. Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi (Amali) (MMA), NACTE (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi), Vituo vyote vya Mafunzo ya Ufundi (Amali) na Taasisi za Zanzibar zinahusishwa kama washirika katika programu hii ya UWwk. Wana majukumu makubwa katika kuwawezesha vijana pamoja na ujuzi muhimu kuingia katika soko la ajira.


Programu ya UWwK imezalisha sanduku la zana kwa masomo mawili ya msingi: Mafunzo na Elimu ya Kuzingatia Umahiri na Maendeleo ya Kazi. Unaweza kupata sanduku zima la zana kwenye mtandao: www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet

**Maendeleo ya Kazi**
Programu ya 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' ikiwemo uchaguzi mpana wa mazoezi ya darasani ambayo husaidia wanafunzi, watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi kupata kuonekana zaidi katika mazingira ya kazi. Kwa kufanya kazi, wote, wale wa ndani ya darasa na nje katika mazingira halisi, vijana hupata habari za hapo kwa hapo kuhusu ulimwengu wa kazi, hufanya kwa vitendo ujuzi tofauti wanaouhitaji kwa ajili ya maendeleo yao ya kazi na hubadilishana uzoefu kwa kila mmoja kati yao. Vipindi vitabuniwa na kutolewa na VMA (Vituo vya Mafunzo ya Amali), Taasisi za Ufundi, Skuli za Sekondari na mashirika mengine ya kiserikali na yasio ya kiserikali, kawaida ni kwa mchango wa wafanya biashara wa ndani (wenyeji). Waajiri na kiongozi (meneja) wa rasilimali watu anaweza kuwa msaada kwa kuwezesha safari za kimasomo, kwa kuwa mkufunzi mgeni wa ndani ya madarasa au kwa kutoa mafunzo ya viwandani.

**Programu ya Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?**

Programu ya Maendeleo ya Kazi huwawezesha walimu wa skuli za sekondari, wakufunzi wa taasisi za mafunzo ya ufundi, kampuni, taasisi zisizo za kiserikali, wizara ya Kazi, Ajira, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Amali) kuchagua mazoezi ambayo yanafaa kwa mahitaji na kiwango cha makundi yao ya vijana.

Programu hailengi kwa vijana kufanyia kazi kwa kujitegemea, bila mwongozo wowote. Bila shaka, washiriki hupata kazi au kazi fulani ya kufanya mmoja mmoja, lakini kwa jumla, hii ni programu ambayo inahitaji mwingiliano, ushirikiano katika makundi na mrejesho. Haiwezi kufuatwa bila mwongozo. Hakikisha unatoa daftari ambalo washiriki wanaweza kuandika na kuhifadhi matokeo na maendeleo yao. Kwenye gamba la daftari, unaweza kuweka mwelekeo wa kazi au washiriki wanaweza kubuni ukurasa wao wa mbele. Walimu na wakufunzi wanahitaji kujiandaa vizuri, na inapendekezwa kwamba mwanzo watafakari maendeleo yao wenyewe ya kazi. Kwa njia hii, walimu na wakufunzi pia ni mfano wa kuigwa katika kuendesha kazi yao wenyewe kiundani.




**Mahiri sita za kazi na dira ya kazi**

Programu 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' imeundwa karibu na mahiri sita ambazo ni muhimu wakati unapotaka kuendeleza kazi yako:

1. Gundua kipaji chako: tafakuri kuhusu uwezo, kupitia umahiri wako mwenyewe kwa heshma ya kazi yako;
2. Gundua shauku yako: tafakuri kuhusu hamasa, kupitia matakwa na maadili yako mwenyewe kwa heshima ya kazi yako;
3. Gundua ulimwengu wako wa kazi: utafutaji wa ajira, mwelekeo kuhusu maadili na umahiri wako kulinganisha na kinachohitajika katika hali ya kazi za kitaaluma;
4. Gundua mtandao wako: mtandao, kufanya na kudumisha mawasiliano ambayo ni muhimu kwa kazi yako;
5. Gundua biashara yako: utafutaji wa ajira binafsi, mwelekeo juu ya matarajio na umahiri wako kuanza biashara au kuendeleza kazi kama mjasiriamali;
6. Mpango kazi wako na kuomba kazi: udhibiti wa kazi, mipango inayohusiana na kazi na ufafanuzi binafsi wa nafasi kwa mchakato wako wa kujifunza na kazi.

Kila umahiri wa kazi umeshikamanishwa sambamba na swala la kazi na jumla ya mahiri sita zinawakilishwa kama usukani wa uendeshaji wa kazi. Unahitaji kuendesha hatua zako za kazi muda wote kutafuta mwelekeo sahihi. Katika maelezo ya kina ya kila moja ya mahiri sita za kazi, unaweza kupata ufafanuzi zaidi kuhusu umahiri unaouhitaji kufanya kwa vitendo, kuendeleza kazi.

**Namna ya kutumia programu kwenye Maendeleo ya Kazi?**
Kila umahiri wa kazi unaweza kufunzwa kwa kufanya mazoezi kadhaa. Mazoezi hutofautiana katika maudhui na katika mbinu pia. Hii ni nzuri, kwa kuwa kuna njia zaidi ya moja ya kujifunza umahiri wa kazi.

Mwanzoni mwa kila mada mpya, utakuta maelezo ya jumla ya mazoezi yote ambayo ni ya mada maalum. Katika maelezo hayo ya jumla, kawaida unakuta: jina cha zoezi, lengo na muhtasari wa mbinu chochezi ambazo zinaweza kutumika katika zoezi hili. Kwa njia hii, unaweza kuangalia kwa haraka mazoezi yote na hii itakusaidia kufanya uchaguzi unaokufaa na kundi lako. Uchaguzi mzuri ni ule unaohusiana na maswala ya maendeleo ya kazi ambao wanafunzi, watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi wanao.

Baada ya kuchunguza maelezo ya jumla, unaweza kuvuta mazoezi uliyochangua. Yote kati yao yana muundo sawa. Kwa njia hii, unaweza kuona kwa urahisi namna ya kuandaa na kutoa zoezi kwa njia inayofaa.

Kwa kufanya uteuzi wako mwenyewe, walimu na wakufunzi wanaweza kubuni programu ya mafunzo. Unachagua mazoezi yale ambayo yanafaa kwa mtaala, ratiba ya vipindi vya kozi na kiwango cha wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi. Uchaguzi unaofanya pia hutegemea na maswali ambayo wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi wanayo kuhusu kazi yao.

Walimu na wakufunzi wanaweza pia kuchagua yale mazoezi wanayopenda kusomeshea. Baadhi ya mazoezi na mbinu zitakufaa zaidi kuliko nyengine. Vidokezo vinavyotolewa mwishoni mwa maelekezo, ni mapendekezo ili kuwezesha zoezi liwe vizuri iwezekanavyo, lakini jisikie huru kulifanya kwa njia tofauti unazodhani zitakufaa au vizuri zaidi kwa kundi lako.

Bila shaka, unaweza kuongeza mazoezi yako mwenyewe kwenye programu hii. Kwa njia hii, sanduku la zana litakua na kwa kubadilishana mazoezi na wengine, mwongozo wa kazi utatolewa kwa njia nzuri zaidi kwa vijana wa Zanzibar na Tanzania.



**Muundo sawa katika mazoezi yote**
Mazoezi yote yanaelezwa kwa kina zaidi, kufuata muundo huo huo. Hii itakusaidia kuandaa na kuwezesha mazoezi uliyoyachagua.

Muundo ni:

**Lengo:** Ni lipi madhumuni ya zoezi? Matokeo gani yatakuwa yanatarajiwa. Kuangalia ufahamu, tabia, ujuzi na vitendo?

**Maandalizi:** Kama mwalimu/mkufunzi, nini cha kufanya katika maendeleo ya kazi kwa ajili ya kutoa zoezi kwa namna ya kuzingatia mchakato? Jinsi ya kuandaa darasa kuwapa washiriki wako eneo wanalohitaji ili kufanya mazoezi? Baadhi ya mazoezi yanahitaji eneo zaidi au mpangilio tofauti wa viti/meza.

**Maelezo:** Kama mwalimu/mkufunzi, nini unaweza kuwaambia wanafunzi/watafutaji wa kazi wako na wabunifu wa kazi kama ni utangulizi kwenye zoezi?

**Utendaji:** Ni nini wanafunzi/watafutaji wa kazi na watoaji wa kazi watalazimika kufanya au kuonesha katika zoezi hilo? Hapa, unaweza kupata mlolongo wa hatua ambazo washiriki huchukua ili kukamilisha zoezi.

**Tafakuri:** Mwaswali gani unauliza mwishoni mwa zoezi (au baada ya hatua mahsusi wakati wa zoezi)?

**Dondoo:** Vitu ambavyo unahitaji kuwa na uelewa navyo wakati wa zoezi.

**Uchunguzi wa kina:** Nini kinaweza kufanywa zaidi kulipa zoezi (kwenda) kina zaidi au kuliunganisha na zoezi jengine?

**Karatasi za mazoezi:** Misaada ya kujifunza, malighafi na vifaa ambavyo vinaweza kutumika na wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi.

# MADA YA 1

**Gundua kipaji chako**
Katika mada ya 1 utakuta mazoezi 20 kuhusu umahiri wa kazi 'Gundua kipaji chako': tafakari kuhusu uwezo.

Gundua kipaji chako inamaanisha: kufikiria kuhusu sifa zako na namna ya kuweza kutumia sifa hizo kuendeleza kazi yako. Wanafunzi, watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi hutafakari juu ya sifa wanazotumia katika maisha yao ya kila siku, skulini na katika kazi (zisizo rasmi). Huwataka wengine (wahitimu, walimu, wanafunzi wenzao, waajiriwa, wajasiriamali na wanafamilia) kuwapa marejesho pale wanapofanya vizuri na pa kuboresha.

Katika maelezo ya jumla ya mada ya 1 unaweza kukuta baadhi ya mazoezi ambapo washiriki watapata kujuana kila mmoja na mazoezi ambapo huchunguza maeneo yao walio na uweledi kwa kutoa na kupata zawadi na mrejesho; kwa kuhojiana kila mmoja na kuwasilisha sifa zao.

Nambari ambayo zoezi hilo linaendana na idadi ya maelezo ya kina ya zoezi hilo na ya karatasi za zoezi. Karatasi za zoezi zinaweza kunakiliwa kwa urahisi kwa ajili ya vijana wako. Hakikisha unatoa daftari ambapo washiriki wanaweza kuandika matokeo yao na wanaweza kuhifadhi matokea na maendeleo yao. Kwenye gamba la daftari, unaweza kuweka dira ya kazi au washiriki wanaweza kubuni ukurasa wao wenyewe wa mbele.

# MAELEZO YA JUMLA YA MAZOEZI 'GUNDUA KIPAJI CHAKO'

| Mazoezi 'Gundua kipaji chako' | Lengo la zoezi | Mbinu shirikishi |
|---|---|---|
| **1.1 Kusimama mstarini** | Zoezi la utangulizi: kufahamiana katika tabia na mada mbalimbali. | Kupanga mstari: kulingana na umri, herufi za kwanza za majina ya familia, vijiji walivyozaliwa au vitu vingine wanavyofanana. Katika kila mstari unaoanza 'majirani' wanapaswa kuwa na mjadala kidogo kuhusu mada hiyo. |
| **1.2 Karibu!** | Zoezi la utangulizi: wakaribishane katika hali ya kimchezo. | Ikiwa katikati ya duara, kila kijana afikiri kuhusu namna atakavyohitaji kukaribishwa katika kundi. Wengine wamkaribishe kijana mwenzao katika namna atakayotaka yeye. |
| **1.3 Naweza kujitambulisha?** | Zoezi la utangulizi: kujifunza namna ya kujitambulisha kwa mtu mwingine au kikundi. | Katika miduara miwili, duara la ndani na duara la nje. Duara moja lijongee katika namna ambayo kila mara mshiriki atakutana na mtu mpya wa kujitambulisha kwake. Baada ya mijongeo mitatu kila mmoja ajitambulishe kwenye kundi. |
| **1.4 Kuvuka mstari** | Zoezi la utangulizi: kufahamiana na kujifunza kuhusiana kwa kupeana taarifa katika hali ya staha. | Katika hali ya ukimya katika kundi, washiriki wenye uzoefu unaofanana (maelezo yatolewe) wavuke mstari na vinginevyo. Kama mkufunzi, unaweza kutoa maelezo yako yanayofaa kundi lako. |
| **1.5 Jina la konani?** | Zoezi la utangulizi: vijana waelezane maana ya majina yao na kwanini wamepewa majina hayo. | Wakiwa wamekaa katika duara, waelezane maana ya majina yao na matukio mengine muhimu kuhusu kuzaliwa kwao. |
| **1.6 Kanuni za dhahabu** | Vijana wajadili kuhusu kanuni na desturi zao na kuzibadilisha kuwa desturi za kikundi, kwa mfano kanuni za dhahabu. | Vijana wajadiliane na kuandaa orodha ya kanuni za dhahabu ambazo vijana wanataka kuziishi darasani. |
| **1.7 Kuelezea kipaji changu katika picha!** | Vijana wagundue jinsi wanavyojisikia wanapozungumzia vipaji na uwezo wao badala ya kuzungumzia mambo ambayo hawayafanyi kwa ufanisi. | Vijana wachague moja kati ya seti ya picha zilizopo mezani ambayo inawakilisha vipaji vyao na katika makundi, waeleze kwanini. |

| | | |
|---|---|---|
| **1.8**<br>**Sikuwa nafahamu kuwa nina kipaji hiki!** | Vijana wagundue vipaji walivyonavyo: zoezi la kutambua sifa walizonazo sio ambazo hawazitambui. | Dakika tano za kuandika orodha yote yavipaji vyao: waandike kwa ukimya. Kama kazi ya nyumbani, waonyeshe orodha hiyo kwa wazazi na rafiki zao na wawaulize mitazamo yao. |
| **1.9**<br>**Asante kwa pongezi!** | Vijana waeleze kuhusu uimara wao, uliotokana na pongezi walizopewa kazini, darasani au nyumbani. | Vijana waorodheshe pongezi tatu na kuelezea ni mazingira yapi ambayo walizipokea. Wanajiuliza kwanini wamefanya vizuri? Wametumia vipaji gani muda huo? |
| **1.10**<br>**Kuponi yangu ya pongezi** | Vijana wapate hisia za namna ya kuomba, kutoa na kupokea pongezi. | Kuponi ya kuomba na kutoa pongezi juu ya vitu vilivyofanywa vizuri na mwanakikundi. Kuwa muwazi. Wanapokea na kutoa pongezi kuhusu mambo ambayo yalitokea katika nyakati halisi na hivi karibuni. |
| **1.11**<br>**Usaili wa vipaji** | Vijana wahojiane mmoja baada ya mwingine kuhusu vipaji vyao na wajifunze namna ya kuwa wawazi. | Wakiwa wawili (au watatu) kwa msaada wa jedwali ambalo wataandika majibu. Aina ya usaili utakaohusisha (hali, zoezi, vitendo na fikra). |
| **1.12**<br>**Vipaji vyangu katika mtazamo wa kihistoria** | Vijana wajiulize swali ni wakati gani au muda ambao walikuza na kutumia vipaji vyao. | Vijana wachore mstari wa kihistoria kuanzia siku yao ya kwanza kwenye mafunzo ya ufundi stadi/ufundi wa viwandani na waorodheshe nyakati nzuri ambazo walitumia na kujivunia vipaji vyao. |
| **1.13**<br>**Nembo yangu!** | Vijana waunde taswira ya utambulisho wao katika picha. | Vijana waandike au kuweka pamoja vipengele vya haiba yao kwenye nembo tupu (sifa, shauku, maadili na ujuzi). |
| **1.14**<br>**Maelezo kwa ufupi: kuelezea ubora wangu ndani ya sekunde 60!** | Vijana wafanye mazoezi ya kutambulisha wasifu wao mbele ya hadhira ndani ya muda mfupi. | Baada ya maandalizi, vijana wote watatoa maelezo mafupi. Wanakikundi watakuwa watazamaji. Kila baada ya simulizi tano kundi jipya la watu watano litaanza kusimulia. Vijana wachukue video kwa simu za kisasa kama zipo. |
| **1.15**<br>**Vipaji vilivyojificha: mwangaza wa mchana!** | Vijana wajizoeshe namna ya kuuliza na kutoa mrejesho kuhusu vipaji vyao vilivyojificha kisha. Watarejea katika vipaji vya wenzao vilivyojificha. | Washiriki watembee darasani wakiwa na karatasi tupu ya A4 migongoni mwao. Kila mmoja awaulize wenzake: 'Je, mnaona vipaji vilivyojificha ndani yangu? Tafadhali viorodheshe'. |
| **1.16**<br>**Vipaji vilivyojificha kwenye kundi letu** | Vijana watafakari kuhusu vipaji vyao wakitumia yale wenzao waliyosema wenzao kuhusu wao. | Seti ya kadi ya chache na kila kadi ikiwa na kipaji au sifa. Namna mbili ya kutumia kadi hizi: kwa jozi, kuchaguliana vipaji vitano au kuchukua kadi moja kati ya hizo na fikiria mtu gani kwenye kundi mwenye kipaji hiki. Elezea kila mara kwanini na katika hali gani. |
| **1.17**<br>**Mtazamo binafsi (selfii)** | Vijana waoneshe wenzao wao ni kina nani kwa kuorodhesha sifa zao na wawape wenzao wasaa wa kuongezea sifa hizo. | Vijana waunde karatasi ya kutundika wenye majina yao na waorodheshe sifa zote walizo nazo. Waweke picha hizi kwenye ukuta. Wanafunzi wenza waruhusiwe kuongeza sifa ambazo wanadhani wenzao wanazo. |
| **1.18**<br>**Hoji kipaji chako** | Vijana wachangie mawazo na mrejesho juu ya vipaji vya wanakikundi wenzao na wapewe mrejesho kuhusu vipaji vyao. | Kwenye vikundi vya watatu watatu A, B na C: wanaotoa, wanaopokea na wanaoandika mrejesho. Badilisha majukumu kila mrejesho mmoja unapotolewa. |
| **1.19**<br>**Shairi la Kitibetan** | Vijana watunge mashairi yao yenye muundo washairi la Kitibetan na waelezee fikra zao za ndani na hisia zao. | Mmoja mmoja, sentensi kwa sentensi, kwa msaada wa mashairi ya Kitibetan yatakayotolewa na mkufunzi, vijana watungeshairi lao. |
| **1.20**<br>**Najivunia...** | Vijana wagundue na kuonesha sifa binafsi na uwezo; watafakari namna ya kufafanua au kuelezea sifa zao. | Kazi binafsi na mahojiano ya jozi, mwisho, hitimisho binafsi liandikwe chini. |

# 1.1 KUSIMAMA MSTARINI

**Lengo**
Vijana watapata kufahamiana katika tabia na mada mbalimbali.

**Maandalizi**
Hakikisha vijana wana nafasi ya kuzunguka na kusimama kwenye mstari. Kwa kina, fikiria kuhusu mada ambazo ungependelea vijana wabadilishane.

**Maelezo**
'Mara nyingi tunakutana kwa kusalimia, kufahamia kwa majina na kujuliana hali. Mbali na hayo tunaweza kuambiana shule ambazo tunasomea au fani zetu ni zipi. Ingawa kuna njia nyingi sana za kufahamiana.'

**Utendaji**
1 Waelekeze vijana kusimama kwenye mstari kulingana na baadhi ya tabia zifuatazo:
- Umri: mwenye umri mdogo zaidi asimame upande wa mbali kushoto, mwenye umri mkubwa zaidi asimame upande wa mbali kulia.
- Jina: kijana mwenye jina linaloanza na herufi A asimame upande wa mbali kushoto na mwenye jina linaloanza na Z asimame upande wa mbali kulia.
- Urefu: kijana mfupi zaidi asimame upande wa mbali kushoto, mrefu zaidi asimame upande wa mbali kulia.
- Jambo alipendalo mtu: mtu ambae jambo analolipenda linaanza na A asimame upande wa mbali kulia.
- Kaka na dada: wasiokuwa na kaka au dada asimame upande wa mbali kushoto, wenye dada na kaka wengi zaidi watasimama upande wambali kulia.
- Mji: anayeishi kwenye mji/kijiji ambacho jina lake linaanza na herufi A asimame upande wa mbali kushoto, anayeishi kwenye mji/kijiji ambacho jina lake linaanza na herufi Z asimame upande wa mbali kulia.
- Chakula pendwa: mtu ambaye chakula anachopendelea zaidi kinaanza na herufi A asimame upande wa mbali kushoto, na yule ambaye chakula anachopendelea zaidi kinaanza na herufi Z asimame upande wa mbali kulia.
- Umbali wa kutoka shuleni kwenda nyumbani: yule ambaye anaishi karibu kabisa na shule yake asimame upande wa mbali kushoto, anayeishi mbali kabisa na shule yake asimame upande mbali kulia.

2 Vijana watakapounda mstari kulingana na moja ya tabia hizo, watawasalimia majirani wa upande wa kushoto kwao na watabadilishana mawazo kuhusu tabia hiyo.
3 Baada ya dakika mbili au tatu za kubadilishana mawazo, waelekeze waunde mstari mwingine kulingana na tabia nyingine iliyochaguliwa na mkufunzi.
4 Rudia zoezi hili hadi utakapounda mistari 4 au 5 tofauti.

**Tafakuri**
Waulize vijana watafakari kuhusu kujitambulisha kwa namna hiyo. Wamegundua vitu ambavyo walikuwa hawafahamu baina yao?

***Dondoo***
Ni vizuri kujadili katika vikao maalumu mada tofauti ambazo unaweza kuchagua kuundia mstari. Weka wazi kitu ambacho unahitaji vijana wafahamu baina yao na kitu gani wanaweza kujifunza kupitia hilo. Kwenye kikao kinachojadili maudhui ya 'familia au jamii' unaweza kuongeza 'taaluma katika familia/jamii yangu' na kuunda mstari kulingana na taaluma za wazazi au watu wengine wa jamii yao. Kisha kijana ambae wazazi/walezi wake wanataaluma zinazoanza na herufi A atasimama upande wa mbali kushoto wa mstari, na yule ambae wazazi wake wanataaluma zinazoanza na herufi Z watasimama upande wa mbali kulia wa mstari.

# 1.2

## Lengo
Vijana wakaribishane katika hali ya kimchezo.

## Maandalizi
Weka viti na meza pembeni, ili vijana wasimame katika mduara. Fikiria wewe binafsi namna tofauti unazoweza kutumia kumkaribisha mtu. Hakuna mipaka. Tofauti na neno 'karibu', kuna njia nyingine maalum za kumkaribisha mtu kwa Zanzibar na Tanzania?

## Maelezo
'Watu hupenda kujisikia wamekaribishwa. Hilo ni hitaji la ndani kabisa la binadamu. Kwanini? Kwa sababu unapojisikia kukaribishwa kuna nafasi ya kujieleza na kufanya mambo ambayo ni muhimu kwako. Unapojiskia kukaribishwa, unaweza kujifunza mengi. Unapojisikia kutokaribishwa, haujisikii huru na huwezi kujifunza. Ni rahisi hivyo. Katika zoezi hili, utakaribishwa kwa namna ambayo unaipenda.'

## Utendaji
1. Muombe kila mmoja atumie dakika moja kufikiria namna ambayo wangependa kukaribishwa kwenye kikundi. Ni muhimu pia wajadiliane katika jozi.
2. Kisha muombe mmoja akuelezeni kwa namna gani angependa kukaribishwa.
3. Waagize washiriki kutoka nje ya darasa/wakae katika duara na lieleze kundi namna mtu huyo anahitaji kukaribishwa.
4. Unaweza kufanya zoezi hili kwa ufupi kuhakikisha kila mmoja anafanya hili kwa usahihi.
5. Omba mshiriki arudi kwenye duara na umkaribishe!
6. Rudia mpaka kila mmoja awe amekaribishwa kwa namna aliyochagua mwenyewe.

# KARIBU!

## Tafakuri
Unafikiria nini kuhusu zoezi hili? Ilikuwaje kusalimiwa kwa namna hii maalum? Wamejisikia kukaribishwa? Ina maana gani kuwa mikusanyiko/mikutano kama hii kwa siku zijazo?

### *Dondoo*
Unapokuwa unafafanua zoezi, unaweza kutoa baadhi ya mifano ya namna ya kukaribishwa. Waachie vijana wafikirie wenyewe namna ambayo wangependa kukaribishwa. Kwa mfano:
- kuingia ndani na kukaribishwa kwa kupigiwa makofi na mishangao kama namna mtu maarufu anavyosalimiwa.
- kuingia ndani ilhali kila mmoja akipiga mluzi kana kwamba wewe ndiye mtu mzuri zaidi duniani.
- kuingia ndani na kupeana tano (salamu) na kila mmoja.
- kuingia ndani na kila mmoja akakwambia 'HABARI<Jina la mwanafunzi>, nimefurahi upo hapo!'
- kuingia ndani huku kila mmoja akikuimbia.

Shiriki zoezi hili: waache wakukaribishe pia.

## Uchunguzi wa kina
Unaweza kuanzisha mjadala na kundi lako wenye maudhui 'ukaribisho' baada ya zoezi hili. Wanajisikiaje kukaribishwa? Ni kitu gani wanahisi ni muhimu wanapofikiria kuhusu 'kukaribishwa'? Wanajisikia kukaribishwa shuleni/kazini? Wanahitaji nini kujisikia wamekaribishwa?

# 1.3 NAWEZA KUJITAMBULISHA?

**Lengo**
Vijana wajifunze kujitambulisha wenyewe kwa mtu mwingine au kwenye kikundi.

**Maandalizi**
Hakikisha una nafasi kubwa ya kupanga viti katika miduara miwili: duara la nje na la ndani. Panga viti katika jozi, vikitazamana weka kulingana na wingi wa washiriki.

**Maelezo**
'Unaweza kujifunza kujitambulisha na kujielezea, hasa kwa kufanya hivyo mara nyingi; unahitaji kufanya mazoezi. Kwanza utajifunza namna ya kujitambulisha kwa mtu mmoja. Mtapangwa kwa jozi na utamwambia mtu mwingine wewe ni nani. Utarudia kujitambulisha kwa wanakikundi wengi kila mara utakapohamisha kiti chako upande wa kulia. Mwisho, utajielezea mwenyewe kwenye kundi zima.'

**Utendaji**
1. Vijana wakae kwenye viti kwenye duara la ndani au la nje. Kila mmoja akae mkabala na mwenzake.
2. Katika jozi, wataelezana wao ni kina nani. Ifupishe: jina lako, umri wako, mahali unapoishi, na nani, kwanini umechagua shule hii, mafunzo haya?, unapendelea nini zaidi?, kitu gani unakiweza zaidi?. Kila swali lina dakika mbili.
3. Baada ya dakika ya nne, washiriki kutoka duara la nje watatoa kiti kimoja na kila mmoja atakaa mkabala na mtu mwingine tofauti sasa. Tutarudia kitu hiki tena: kila mmoja katika jozi ana dakika mbili kujitambulisha kwa mwenzake aliyekaa mbele yake.
4. Kisha tutafanya hivyo mara moja zaidi; washiriki wote kutoka duara la nje watahama sehemu moja tena na kila mmoja atajitambulisha kwa mtu mpya aliyekaa mkabala nae.
5. Hatimaye, kila mmoja atapata zamu ya kujitambulisha kwenye kundi zima. Mwanafunzi ambaye itakuwa zamu yake, atasimama, atawatazama watu wote kwenye kikundi, atatumia muda wake kujielezea.
6. Akimaliza, ataendelea kusimama kwa muda na kisha kukaa chini kimyakimya.
7. Rudia zoezi hili mpaka kila mmoja atakapofikiwa.

**Tafakuri**
Waulize vijana wanafikiria nini? Wameiona hii kuwa njia nzuri ya kufahamiana zaidi? Kwa upande wao nini tofauti baina ya kujitambulisha kwa mtu mmoja dhidi ya kujitambulisha kwenye kikundi? Wamepata nini kupitia zoezi hili? Watapenda kufanya kitu gani tofauti wakati mwingine? Kitu gani watafanya vile vile? Hakikisha kuna awamu nyingine.

***Dondoo***
Usiwapangie zamu, ila waache vijana wachague namna ya kuhakikisha kila mmoja anapata zamu yake. Anaependa kufanya zoezi hili, ni mfano kwa wengine.

# 1.4 KUVUKA MSTARI

**Lengo**
Vijana wapate kufahamiana na kujifunza kutegemeana kwa kupeana taarifa katika hali ya staha.

**Maandalizi**
Ondoa meza na viti kwenye chumba. Hakikisha kuna chumba kikubwa kuweza kutembea. Kwa kutumia kamba, chora mstari katikati ya chumba. Andaa maelezo ambayo unahitaji kutumia.

**Maelezo**
'Kitu kizuri kuhusu kikundi ni kuwa kikundi kinajumuisha watu tofauti wenye mahitaji na historia tofauti. Kuna mambo mengine ya kujifunza baina yao. Ila tambua, ni muhimu kujisikia salama, kwa sababu bila usalama haiwezekani kujifunza. Unajenga usalama pale unapomfanya mwenzako apate hisia kuwa una mkubali. Wakubali wengine kama walivyo ni muhimu baadaye katika mazingira ya kazi, pale ambapo hautakuwa na uwezo wa kuchagua mwenzako. Katika zoezi hili 'kuvuka mstari' tutajaribu namna ya kufahamiana vizuri kwa kupeana taarifa binafsi katika mazingira salama. Zipo kanuni mbili:

- Kaa kimya wakati wa zoezi
- Kila litakalozungumzwa au kuoneshwa litabaki kuwa siri yetu.'

**Utendaji**
1. Soma kwa sauti -mmoja baada ya mwingine- chaguo lako kati ya maelezo yafuatayo.
2. Maelezo haya ya takapotolewa na mshiriki, atavuka mstari.
3. Vijana wasimame na kugeuka kutazama ni nani kavuka mstari pamoja nao.
4. Baada ya hapo, vijana wataweza kurudi mahali pao pa awali.
5. Hakuna atakaeongea wakati zoezi likiendelea.

**Sentensi:**
- Ninatakiwa kusafiri zaidi ya saa moja kufika shuleni.
- Nimechagua mafunzo haya kwa sababu nimeambiwa hivyo na wazazi wangu.
- Nimechagua mafunzo haya kwa sababu sikuwa nafahamu kitu gani ninahitaji.
- Nimechagua mafunzo haya kwa sababu ninahitaji kweli kufanya kazi hii.
- Nimechagua mafunzo haya kwa sababu marafiki zangu walikuwa hapa.
- Huwa ninajisikia vibaya ninapoamka asubuhi.
- Ninapata shida kupata muda wa kufanya kazi zangu za nyumbani.
- Kuna wakati ninahisi sipo salama.
- Nilikuwa nahofu kiasi siku yangu ya kwanza shuleni.
- Ninapata shida kufundishwa kwa lugha ya Kiingereza.
- Sina pesa yakutosha kununua kifungua kinywa asubuhi.
- Wazazi wangu wametalikiana.
- Nimepoteza mtu wa karibu sana na mimi.
- Nimedanganywa.
- Mwalimu anapofundisha kwa zaidi ya saa moja, napata shida kuendelea kumsikiliza.

Hauhitaji kutumia maelezo yote hapo juu. Fanya chaguo lako na fikiria kuhusu maelezo mengine ambayo yatawafaa vijana wa kundi lako na utamaduni wa Zanzibar na Tanzania bara.

**Tafakuri**
Uliza kundi lako namna gani wangependa kufanya zoezi hili. Wamegundua nini? Kuna mambo ambayo hawakufahamu kabla? Kuna mambo ambayo wangehitaji kumwambia mtu fulani baadaye, kwa sababu ya zoezi hili?

***Dondoo***

Shiriki zoezi hili, itakufanya uwe mfano kwa vijana na itaongeza uaminifu. Hakikisha washiriki ambao hawaongei sana, wanafikiwa na waulize kwa kina namna gani wamejifunza kutokana na zoezi hili.
Fikiria kufanya zoezi endapo unahisi kundi haliko salama kufanya zoezi. Labda kundi linahitaji mazoezi ya utangulizi zaidi ili kuwa tayari kwa zoezi la 'kuvuka mstari'. Kama unahisi kundi liko tayari na mazingira yako salama, ni vyema kufanya zoezi pamoja na wenzako. Huwezijua labda baadhi ya maelezo yanaweza kuibua hisia kali sana. Endapo itatokea: inaweza kuwa rahisi endapo wenzako watakuwa makini kwenye kundi, wakati ukimsaidia kijana mmoja au kinyume chake.

# 1.5 JINA LAKO NANI?

**Lengo**
Vijana waelezane maana ya majina yao na kwanini wamepewa majina hayo.

**Maandalizi**
Kabla hujafanya zoezi hili waelekeze vijana wachukue alama ya namna wazazi wao wanavyosherehekea siku za kuzaliwa kwao, ili waweze kuelezea kitu kuhusu hilo. Vijana ambao hawana kitu maalum cha kuonesha, wanaweza kuleta picha ya enzi wanazaliwa, au waandike majina yao kwenye kadi/kipande cha karatasi kwa herufi nzuri. Weka vyote katika mduara; hakuna meza, ili kila mmoja aweze kumuona mwenzake. Lete alama hiyo mwenyewe, ili uweze kuwa mfano wa kuigwa kwenye darasa.

**Maelezo**
'Wote tumezaliwa kwenye familia, nchi na kijiji kwa wakati fulani. Hicho ndio kitu tulichonacho kwa pamoja. Hakuna ambaye hili halimuhusu. Na pia, kila uzao ni wa pekee. Na ndio maana uzao unahusishwa na ibada za asili kwenye nchi nyingi. Kama ilivyo kwenye baadhi ya nchini desturi yao kutuma taarifa za uzazi. Marekani wana 'baby shower' tafrija ya kusherehekea kuzaliwa kwa mtoto. Katika baadhi ya nchi, mtoto hutahiriwa na mahali pengine mtoto huanzishwa maisha na mtu anayeaminika kuwa na hekima. Katika zoezi hili, tutachambua zaidi kuhusu majina yetu na mila gani huchukua hatamu wakati wa kuzaliwa kwetu.'

**Utendaji**
1. Waelekeze vijana waweke chini alama/picha/jina yao katikati ya duara.
2. Alama/picha/jina moja baada ya jingine lichukuliwe na mshiriki aombwe kueleza inawakilisha nini, maana ya majina yao na kwanini walipewa majina hayo.
3. Waulize vijana ni matambiko na tamaduni gani zinazofanyika wakati mtoto anapozaliwa kwenye maeneo wanayotokea.

**Tafakuri**
Waulize vijana wanajisikiaje kuyajadili majina yao na maana zake katika kundi? Je, wamegundua vitu kwenye majina, mila na alama za wengine ambazo hawakuwa wakifahamu kabla?

***Dondoo***
Endapo kundi ni kubwa sana, ligawe kundi katika vikundi vidogo na waelekeze wafanye hivyo hivyo. Waache waandike majina yote na maana zake yaweze kujadiliwa baadaye na kundi.

# 1.6 KANUNI ZA DHAHABU

**Lengo**
Vijana wajadili kuhusu kanuni na desturi zao na kuzibadilisha kuwa desturi za kikundi, kwa mfano kanuni za dhahabu.

**Maandalizi**
Hakikisha kila mmoja ana kalamu na karatasi ambayo haina maandishi. Unahitaji pia kalamu ya wino mzito, ubao mweupe/karatasi kubwa la kuandikia na bango (au kipande kikubwa cha karatasi) kuandikia kanuni za dhahabu.

**Maelezo**
'Ni kanuni zipi za dhahabu ambazo ni muhimu kwenye kundi letu? Ni tabia gani tunadhani zitasaidia kufanya kazi pamoja na kujifunza vizuri? Ni masuala gani yanatakiwa na yapi yasiyotakiwa kufanyika darasani? Kanuni zetu binafsi ni zipi? Hivi ndio tutajifunza katika kipindi hiki. Usomaji wa darasani utaongezeka, endapo tutaishi na kanuni hizo za dhahabu; vitu ambavyo binafsi tunavithamini, vitakuwa kanuni za kundi letu. Kanuni kumi za dhahabu zitaandikwa kwenye bango (au kipande kikubwa cha karatasi), ili tuweze kuziona wakati wote.'

**Utendaji**
1. Anza na utangulizi kwanini kanuni za dhahabu ni muhimu. Sisitiza kuwa kanuni za dhahabu zinatakiwa kueleweka kwa kila mtu. Waambie kila kitakachojadiliwa kitabaki kuwa siri ya kikundi, isipokuwa kama kundi litaamua tofauti. Hii inaweka usalama kwenye kundi.
2. Kila mmoja, na wewe pia, aandike kanuni zake tano muhimu zaidi za dhahabu na kwa maneno machache aongeze, kitu ambacho kila kanuni inamaanisha kwake.
3. Waache wajadili kanuni zao binafsi na maana zake kwenye makundi madogo ya washiriki watano. Baada ya hapo, waelekeze kuandaa orodha moja ya kanuni kumi.
4. Andika kanuni za vikundi vidogo kwenye ubao au ubao mdogo (sikiliza kinachozungumzwa na andika maelezo yote bila kuchangia kitu). Kila mshiriki wa kikundi kidogo atapata nafasi. Endapo mmoja wao tayari ameshaitaja kanuni, weka alama karibu na kanuni hiyo.
5. Jadiliana na kikundi ni zipi kati ya kanuni zilizopo ubaoni zinaweza kuwekwa kwenye orodha ya kanuni kumi muhimu zaidi za dhahabu.
6. Usipotoshwe na kanuni iliyopata kura nyingi. Sikiliza kundi, sikiliza maana hasa ya tabia zilizopendekezwa, sikiliza majadiliano ya hoja na chagua kilicho muhimu zaidi.

**Tafakuri**
Waulize vijana wamejisikia vipi kuhusu hali ya kikundi wakati wa zoezi. Kila mmoja amepata nafasi ya kuchangia mawazo? Uliza wanafunzi wachache endapo kanuni/taratibu zao zilikuwa na mfanano na za wengine? Wanadhani itakuwa ngumu kufuata kanuni hizi za dhahabu? Vijana watafanya nini endapo wengine hawatafuata kanuni hizi? Watafanya chochote kuhusu hili? Baada ya makubaliano na kila mtu ndani ya kundi kuhusu kumi bora, kanuni zitawekwa kwenye utendaji.

***Dondoo***
Jiepushe na mijadala mirefu ambayo ni ngumu kuisitisha. Hakikisha hakuna kutokukubaliana kwenye baadhi ya kanuni na usiongeze kanuni zako kwenye kundi. Kubaliana na makubaliano ya jumla.

**Uchunguzi wa kina**
Itakubidi, au kwa ufafanuzi, unaweza kujadili kanuni za dhahabu baadae kwenye kozi tena; hii unafanya ili kutathmini endapo vijana wanaheshimu kanuni na endapo kanuni zinahitaji kuboreshwa/kubadilishwa. Hakikisha unawapa pongezi pale ambapo watakuwa sahihi. Fanya hivi pia wakati ukiwa unafundisha.

# 1.7 KUELEZEA KIPAJI CHANGU KATIKA PICHA!

**Lengo**
Vijana wagundue jinsi wanavyojisikia wanapozungumzia vipaji na uwezo wao badala ya kuzungumzia mambo ambayo hawayafanyi kwa ufanisi.

**Maandalizi**
Weka pamoja kadi za kutoka Tanzania bara, Zanzibar au Afrika katika kipaji au ubora ambao watu wameonesha. Unaweza pia kuwaambia vijana watengeneze picha ambazo kwazo wataonesha vipaji vyao/ubora wao. Panga viti katika mduara, weka kadi na picha katikati ya duara kwenye sakafu ili vijana waweze kusimama/kutembea pembeni yake. Hakikisha sakafu ni safi, kama sio safi, weka meza katikati ya duara na weka picha na kadi juu ya meza.

**Maelezo**
Inatokea mara nyingi sana tunatazama mambo ambayo hatuyawezi vizuri. Katika zoezi hili, tutaangalia kile ambacho tunaweza kufanya vizuri. Sote tutaoneshana yale ambayo tunayawezana tutafanya hivyo kwa kuchagua picha ambayo tunadhani inatufaa vizuri.'

**Utendaji**
1 Kila mmoja achague kadi au picha ambayo kwayo ataweza kugundua kipaji/wasifu wake.
2 Kila mmoja apate nafasi ya kuwaelezawengine kwanini amechagua kadi/picha hiyo na kwa namna gani inaelezea vipaji vyao.
3 Wanakikundi wengine waulize maswali kuhusu yale wanayoelezwa na mwenzao.

**Tafakuri**
Waulize vijana walijisikiaje kuhusu kuwa makini kwenye vipaji na uwezo. Wanajisikiaje kulizungumzia hilo? Wamezoea kuzungumzia yale ambayo wanayamudu? Wamejifunza kitu kutokana na mapokeo ya wenzao? Kama ndio, wamejifunza nini?

***Dondoo***

Hakikisha vijana wanapata usikivu sawa ili kuelezea na kuweka wazi vipaji vyao. Endapo vijana watakuwa na uzoefu mdogo wa kuelezea vipaji vyao, katika hali hii zoezi hili litakuwa gumu kwao. Ikiwa hivyo, itakuwa vizuri kama ukishiriki katika zoezi hili na ulieleze kundi kwanini umechagua kadi hiyo. Ni vyema kufanya zoezi hili katika nyakati tofauti ndani ya mwaka. Kisha uliza kundi kitu walichogundua kuhusu vipaji/uwezo hivi karibuni.

**Uchunguzi wa kina**
Wakati unafanya zoezi hili - au linalofanana na hili - mara nyingi utagundua kwamba vijana wamezoea kuzungumzia uwezo badala ya udhaifu. Kama mkufunzi, unatakiwa kuzungumzia vipaji na sio kuhusu udhaifu tu. Kama zoezi hili likitumiwa mara nyingi, vijana watagundua uwezo wakutaja uwezo wao na kugundua vipaji vyao unaongezeka.

1.8

# SIKU WANAFAHAMU KUWA NINA KIPAJI HIKI!

**Lengo**
Vijana wagundue vipaji walivyonavyo: zoezi la kutambua sifa walizonazo sio ambazo hawazitambui.

**Maandalizi**
Andaa zoezi hili kwa kulifanya mwenyewe. Kwanza andika kwa dakika 5 kitu unachokiweza zaidi. Weka kengele na tumia dakika tano kamili, hata kama una dhani hakuna chochote unachoweza kuongeza. Huwa kuna nafasi unafikiri zaidi kuhusu kitu fulani. Kwa kufanya zoezi hili mwenyewe, utaweza kugundua kitu gani kitakuwa kigumu kwa washiriki wako katika zoezi hili. Hakikisha kila mmoja ana karatasi na kalamu.

**Maelezo**
'Tunaenda kuandika kitu ambacho tunakiweza zaidi, na tutatumia muda wetu kufanya hilo. Utapata dakika tano za kuandika kila kitu unachofikiria. Na tutatumia kila sekunde ya hizo dakika 5, hata kama hudhani kama unaweza kuibuka na kitu kipya. Huruhusiwi kuongea ndani ya hizi dakika 5.'

**Utendaji**
1. Waeleze washiriki wako waandike vitu ambavyo wanaviweza zaidi. Si lazima waandike kwa sentensi kamili; haitakiwi kuwa simulizi. Andika, andika, andika bila kujiuliza kama uandishi ni mzuri wa kutosha. Andika bila kutoa kalamu yako kwenye karatasi! Andika kile kinachokuja kwenye kichwa chako kuhusu vipaji vyako.
2. Eleza kundi lako mara tu dakika tano zikianza, hakikisha kila mmoja yupo kimya na kwamba mtunza muda atatangaza mwisho wa zoezi.
3. Kengele ikigonga tu zoezi limeisha, wape muda wa kupumzika kidogo. Mara nyingi wataanza kucheka na kuongea.
4. Waeleze vijana wasome kwa sauti yale waliyoandika na kujifunza kutokana na hili. Kitu gani kipya?

**Tafakuri**
Waulize vijana nini wamejifunza wakati wa zoezi hili? Ilikuwaje kuvipa vipaji vyao muda wa kuvifikiria? Wamegundua mambo yaliyowashangaza? Kama ndivyo, mambo yapi?

***Dondoo***
Endapo vijana itawawia vigumu kuandika chochote, waeleze kufikiria nyakati ambazo walipata pongezi, walipofanya vitu ambavyo walijivunia wakati wa kutatua tatizo. Ni jambo gani walifanya vizuri katika hali hiyo? Hicho ndicho wanatakiwa kuandika. Ni muhimu sana kulifanya zoezi lidumu kwa dakika 5. Inachukua muda kupata taarifa kutoka kwenye kichwa kisichojua chochote.

**Uchunguzi wa kina**
Waeleze vijana kuwapatia marafiki au wazazi wao wasome yale waliyoandika. Mkutano/kipindi kijacho waulize ni namna gani marafiki/wazazi wao walipokea. Unaweza kurudia zoezi hili baadae kwa muundo tofauti, kwa mfano: 'Tumia dakika 5 kuandika namna gani maisha yatakuwa baada ya miaka 5' au 'Tumia dakika 5 kuandika namna gani kazi unayoipenda itakuwa' au 'Tumia dakika 5 kuelezea shule/mafunzo yako bora'.

# 1.9 ASANTE KWA PONGEZI!

**Lengo**
Vijana waeleze kuhusu uimara wao, uliotokana na pongezi walizopewa kazini, darasani au nyumbani.

**Maandalizi**
Maandalizi bora kabisa ya zoezi hili ni kulifanya mwenyewe kwanza. Andika uimara wako na pongezi ulizopewa kutoka kwa wengine. Kwa namna hii utajifunza kitu ambacho kundi lako litaona ni kigumu kwenye zoezi hili na utaonekana kama mfano.

**Maelezo**
'Tunaelekea kutazamia uimara wetu kwa kusikiliza yale wanayosema wengine kuhusu sisi. Tunapokea pongezi gani? Watu wanatuambia nini pale wanapozungumza mazuri kuhusu sisi? Kulinganana na mtazamo wa wengine tunaweza nini? Wakati mwingine inatuwia vigumu kupokea pongezi, lakini mara nyingi wanakuwa na hoja.'

**Utendaji**
1. Waelekeze vijana waandike angalau pongezi 3 ambazo wamewahi kupokea hapo nyuma. Pongezi hizo zitakuwa zinahusiana na elimu, kazi au maisha yao binafsi.
2. Waache waandike aina ya kazi walizofanya mpaka kupokea pongezi hizo.
3. Baada ya hapo waambie wafafanue tukio 1 kati ya 2 ya hivi karibuni ambayo huwa wanajivunia na waliyafanya kwa mafanikio. Nini kiliwapa nguvu? Kitu gani kilifanya tukio hilo kuwa maalum sana kwao (na watu wanaowazunguka)? Ni vipaji/sifa gani walizotumia katika matukio hayo?
4. Waambie vijana kujadili matukio haya ya hivi karibuni na majirani zao.

**Tafakuri**
Tafakari na vijana namna walivyojisikia walipopongezwa. Wanapata tabu kuzikumbuka pongezi? Je, ndani ya familia yako, shuleni, kwenye kundi la marafiki zako kuna tabia ya kupeana pongezi? Ndiyo, kwanini? Hapana, kwanini? Ni wazo gani, thamani ipi iliyopo nyuma ya hili?

***Dondoo***
Kama vijana watapata shida kufikiria kitu cha kuandika, wapongeze kwa nafasi yako kama mkufunzi. Waambie waandike pongezi hiyo na baada ya hapo wajibu maswali mengine. Au omba mshiriki mwingine ampongeze mwenzake.

**Uchunguzi wa kina**
Kama mkufunzi, jenga tabia ya kutoa pongezi. Na unaweza kurudia zoezi hili kwa namna tofauti: mara moja ndani ya wiki kadhaa, waache vijana wapeane pongezi au kila kijana achague wenzake watatu atakaowapa pongezi ili kuhakikisha kila mmoja kwenye kundi anatoa na kupokea pongezi, hivyo utahitaji kupanga nani atampongeza nani.

# 1.10

# KUPONI YANGU YA PONGEZI

KARATASI YA ZOEZI 1.10

**Lengo**
Vijana wapate hisia za namna ya kuomba, kutoa na kupokea pongezi.

**Maandalizi**
Hakikisha umechapa kuponi za pongezi za kutosha kugawa: moja au mbili kwa kila mmoja. Unaweza kuchapa kuponi kutoka karatasi ya zoezi 1.10 'Kuponi yangu ya pongezi'. Jaza moja ya kuponi hizo mwenyewe ili kugundua kitu ambacho vijana watapata shida kufanya.

**Maelezo**
'Tunaelekea kujifunza kuhusu pongezi: namna ya kuomba, kutoa na kupokea pongezi. Pongezi ni muundo wa mrejesho ambao utakufurahisha na kupitia kwake utagundua kitu ambacho unakimudu au kitua mbacho watu wanadhani ni bora kuhusu wewe. Unapomsifia mtu, ni muhimu uwe unamaanisha kile unachokisema na uwe bayana kuhusu kitu unachodhani kuwa nguvu ya mtu fulani iko katika uhalisia.'

**Utendaji**
1 Waelekeze vijana kuandika majina kwenye kuponi zao kisha wampatie yeyote kwenye kundi ambae wangependa kupokea pongezi kutoka kwake. Wao pia wapokee pongezi kutoka kwa mtu mwingine pia. Waombe pongezi mara tu watakapotoa kuponi.
2 Baada ya hapo kila mmoja atajaza ujumbe kwenye vocha. Waeleze wafikirie mambo mazuri ambayo wanaona kwa mwenzao na wawe wazi kadri ya uwezo. Acha watoe pongezi, waandike kwa maneno machache, na ikiwezekana watumie mifano. Waache watie saini za majina yao kwenye kuponi.
3 Endapo yote yamefanyika, kila mmoja arudishe kuponi na kumpongeza mwenzake kwa maneno.

**Tafakuri**
Tafakari na vijana ni namna gani walimudu pongezi wakati wa zoezi hili. Walipata shida kupokea pongezi? Walipata shida kutoa pongezi? Wamejisikia vipi pale wanapopokea pongezi nzuri kutoka kwa mtu fulani? Wanaamini hizo ni pongezi za kweli? Ni wakati gani wanapata shida kutoa pongezi? Wanaweza kufikiria kuhusu watu ambao kamwe hawawezi kuwapa pongezi?

***Dondoo***
Endapo itatokea, pongezi zikaombwa kutoka kwa baadhi ya wanafunzi tu, weka ukomo kwa hilo. Kwa mfano: unaweza kutoa pongezi kwa wanadarasa wawili/kujaza kuponi mbili. Mtu atakayejaza kuponi mbili anatakiwa kuomba kuponi mbili pia kutoka kwa wanadarasa wenzake pia. Hizo kuponi za ziada zitajazwa na mwingine ambaye hajapokea kuponi kutoka kwa mwanafunzi mwenzake. Hivyo, hakikisha vijana wote wanatoa pongezi. Sio rahisi kwa watu kupokea pongezi. Tambua hilo na waeleze wanafunzi kuwa kimya kwa muda baada ya kuwa wamepewa pongezi. Wakati mwingine pongezi huwa zinachekwa, au kujadiliwa kitu ambacho kinapunguza thamani yake.

**Uchunguzi wa kina**
Kama mkufunzi, jenga tabia ya kutoa pongezi. Au rudia zoezi hili kwa namna nyingine: vijana waunde duara wakati wa kutafakari kuhusu zoezi hili, kwa nafasi yake kila mmoja aeleze kitu gani amejifunza. Kisha wageuke upande wao wa kulia/kushoto kuwatazama majirani zao na wawape pongezi kwa mchango wao kwenye mkutano huu.

# 1.11

# USAILI WA VIPAJI

KARATASI YA ZOEZI 1.11

**Lengo**
Vijana wahojiane mmoja baada ya mwingine kuhusu vipaji vyao na wajifunze namna ya kuwa wawazi.

**Maandalizi**
Jaza ratiba hiyo mwenyewe pia, ili uweze kujibu maswali ambayo wanafunzi watakuwa nayo. Weka meza na viti kwenye vikundi vya watu watatu. Hakikisha una vifaa vya kuwatosha wanafunzi wote. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 1.11 'Usaili wa vipaji' au andika maswali katika ubao. Washiriki/wanafunzi wanaweza kutumia daftari au karatasi tupu za A4.

**Maelezo**
'Tunakwenda kuhojiana wenyewe kuhusu vipaji vyetu. Ni muhimu sana ukisikiliza kwa makini mambo anayosema mtu mwingine, utakachoandika kiendane na kile kilichosemwa, bila kuongeza mawazo yako. Kisha mueleze mwingine kipaji chake ni kipi kulingana na dodoso ulilojaza wakati wa usaili.'

**Utendaji**
1. Gawanya kundi la watu watatu watatu.
2. Toa mfano wa usaili kwenye karatasi ya zoezi 1.11 'Usaili wa vipaji'.
3. Waeleze vijana kuhojiana na kuandika majibu yao kwenye modeli. A msailiwa, B msaili na C anaandika majibu. Badilisha majukumu baada ya usaili kuisha.
4. Usaili utapomalizika, waambie vijana watambulishe vipaji vya wenzao kwa wanakikundi wenzao.

**Tafakuri**
Tafakari kwa ufupi namna gani vijana wameelewa aina hii ya usaili. Wamejifunza nini kuhusu wengine ambao hawakuwa wakiwatambua kabla? Wamejifunza nini kwa kuelezea vipaji vyao wenyewe?

***Dondoo***

Fafanua kwa wanafunzi kuwa changamoto kubwa ya kumfanyia mtu usaili ni kusikiliza kwa umakini bila kuhukumu yale unayoambiwa. Ni muhimu kumpa mtu nafasi ya kutoa hadithi yake na kujifunza kutokana na hadithi hiyo.

**Uchunguzi wa kina**
Waachie vijana wawahoji wazazi wao au mtu mwingine kwenye kampuni. Itakuwa msaada kwao kupata mwanga kupitia vipaji vya wengine.

1.12

# VIPAJI VYANGU KATIKA MTAZAMO WA KIHISTORIA

**Lengo**
Vijana wajiulize swali ni wakati gani au muda ambao walikuza au kutumia vipaji vyao.

**Maandalizi**
Chukua karatasi kadhaa (za A4) na penseli za rangi/kalamu za wino mzito, za kutosha idadi ya washiriki. Panga meza zote katika umbo la mraba, ili wanakikundi waweze kutazamana.

**Maelezo**
'Tunahitaji kujizoesha kuongelea mambo ambayo yalifanyika vizuri. Hasa hasa shuleni, kila mara huwa tunaongelea mambo ambayo hayakwenda vizuri na tunahitaji kubadilika. Tuna mashaka kuwa hilo linatuhamasisha kufanya mambo kwa utofauti. Mbadala mwingine ni kuzungumzia mambo ambayo tunayaweza. Hili litatufanya tuwe na furaha na kutushawishi kujaribu kufanya vitu fulani kwa namna tofauti. Hicho ndicho tutafanya kwenye zoezi hili.'

**Utendaji**
1 Waache vijana wachukue kipande cha karatasi na waeleze wachore mstari wa kihistoria kuanzia siku ya kwanza ya kuanzakozi/masomo ya viwandani mpaka leo.
2 Waelekeze wachore au kuandika kwenye mstari huo kama watakuwa na mtazamo chanya:
   - lini ulikuwa mahali pako?
   - lini ulikuwa unafanya kitu unachokiweza?
   - lini ulijisikia fahari?
3 Waelekeze waandike:
   - walikuwa wanafanya nini nyakati hizo?
   - walitumia vipaji gani?
   - kitu gani walikuwa wanakiweza vizuri na lini walifurahia kutenda?
   - ni katika aina ipi ya mazingira, walipiga hatua (katika majukumu yapi, watu gani, mazingira yapi: shuleni, nyumbani, kazini au na wazazi)?
4 Wapange vijana katika jozi na waambie waelezane vitu gani wamechora na kuandika. Mistari yao itaeleweka vipi?

**Tafakuri**
Wakati wa tafakuri ya kundi, waulize nani anahitaji kushirikisha kundi mstari wake. Uliza kikundi wanafikiria nini kutizama vipaji vyao kwa namna hii. Ni hitimisho gani linaweza kufikiwa baada ya zoezi hili. Wanaweza kufikiria kuhusu vitu ambavyo wangependa kufanya tofauti wakati ujao? Au watarudia hivi kama awali?

***Dondoo***
Unda mstari wako wa historia, ili uweze kutambua mambo ambayo vijana yanaweza kuwapa changamoto na uweze kujibu maswali yao. Mistari yote ya kihistoria ni bora. Hakuna mstari mbaya: kila mtu kwa namna yake amepitia uzoefu fulani hapo nyuma. Tazama kila mchoro kwa nidhamu. Kufikiria kuhusu tabia yako kwa namna hii, ni zoezi gumu kufanya.

**Uchunguzi wa kina**
Rudia zoezi hili mara nyingi kipindi cha mwakawa masomo. Vijana watajifunza kuangalia kwa mtitiriko tabia zao na watagundua mabadiliko ambayo wamepitia. Kwa kulinganisha mstari wa kihistoria mpya na wa zamani, wataweza kuweka ukuaji wao katika maneno.

# NEMBO YANGU!



**Lengo**
Vijana waunde taswira ya utambulisho wao katika picha.

**Maandalizi**
Kuandaa zoezi hili unaweza kuchukua picha chache/nembo ya Zanzibar au ya kwenye mji wenu. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 1.13 'Nembo yangu' au chora moja katika bango la chati mgeuzo. Kusanya magazeti ya kutosha na vitendea kazi kama karatasi, mkasi, kalamu za wino na karatasi gundi.

**Maelezo**
'Hapo nyuma, kwa mfano nembo ya Sultan ilionesha kile ilichowakilisha, familia aliyotokea. Majiji, watukufu au familia ya Sultan wote wana nembo ambazo mpaka leo bado zinatumika. Mfano, hata hapa Tanzania kuna nembo ya bibi na bwana ambayo inaonesha na kuuwakilisha utanzania halisi na fahari zilizopo Tanzania kama ndovu. Utaunda nembo yako leo, itaonesha wewe ni nani. Itajumuisha taarifa muhimu kuhusu wewe.'




**Utendaji**
1 Gawa karatasi ya zoezi 1.13 'Nembo yangu' na nembo tupu kwa kila mmoja. Waulize vijana ni namna gani wangependa kujielezea kwa dunia nzima kwa kuweka alama kwenye nembo zao, kutumia maandishi, picha au michoro. Wao ni kina nani? Ni kitu muhimu kwao? Ni kitu gani kinawafurahisha?
2 Vijana watabandika nembo kwenye ukuta wa darasa na wataangaliana uwasilishaji wao.
3 Kila mtu atapata wasaa wa kuielezea nembo yake mbele ya darasa na kufafanua maana yake na inaelezea nini kuhusu yeye.
4 Waambie vijana wapige picha/wajipige picha na nembo zao.

**Tafakuri**
Waulize vijana kama wamefurahia mtazamo wao binafsi. Je wameweza kuelezea yale ambayo walitaka kuelezea? Uliza majibu kutoka kwa wanafunzi wengine: wanadhani kuwa nembo hiyo inamuwakilisha mtu aliye itengeneza? Kuhitimisha: wamependa nini kwenye zoezi hili?

***Dondoo***
Utakapohitaji kuunda nembo kubwa unaweza kuwapatia washiriki karatasi kubwa. Kwanza ichore kazi hiyo kwenye ubao au kwenye karatasi kubwa kama mfano kisha waambie vijana wainakili kwenye karatasi zao.

# 1.14

# MAELEZO KWA UFUPI: KUELEZEA UBORA WANGU NDANI YA SEKUNDE 60

**Lengo**
Vijana wafanye mazoezi ya kutambulisha wasifu wao mbele ya hadhira ndani ya muda mfupi.

**Maandalizi**
Kuwaandaa vijana kwa ajili ya zoezi hili, wapatie baadhi ya maswali ya kujibu kama kazi ya nyumbani (kama wiki moja). Swali unaloweza kuwauliza kwa mfano ni, endapo nikimuuliza baba yako au mama yako (au kaka/dada/rafiki) kitu gani wewe unakiweza, watanijibu nini? Au unaweza kuwapatia vijana orodha ifuatayo ya maswali kujibu:

- Mimi ni nani?
- Nguvu yangu ni ipi?
- Ni kitu gani ninakiona muhimu katika maisha yangu?
- Ni kitu gani ninakiweza vizuri?
- Ninahitaji kutimiza nini?
- Kitu gani kinanifanya niwe maalumu?

Waeleze vijana waandae maelezo mafupi ya sekunde 60 kulingana na majibu ambayo wameandaa. Maandalizi kwa ajili ya maelezo mafupi: hakikisha darasa limeandaliwa kwa ajili ya uwasilishaji. Viti pekee, usiweke meza. Fikiria ni kwa namna gani ungependa vijana wawasilishe maelezo yao mafupi. Kwa mfano: kupeana zamu mvulana/msichana, mmoja ajitolee kwenda kwanza na liache kundi lichague nani atafuata, au mmoja aende kwanza kisha achague nani anafuata, n.k.

**Maelezo**
'Makampuni mengi siku hizi yanatumia kitu kinachoitwa 'maelezo kwa ufupi'. Hii ni mbinu ya kujielezea ndani ya sekunde 60, kwa mfano watu wa kwenye kamati ya usaili. Sababu ya msingi ya maelezo ya haraka ni kwamba, ni kama vile unaongea na mwenzako ambaye amesimama karibu yako kwenye lifti. Hakuna mambo mengi ya kuongea. Fikiria kwamba unahitaji kitu kutoka kwa mtu huyo na unataka awe makini na wewe. Mwenzako anaenda ghorofa ya 10, inamaanisha una ghorofa 10 kuibua utashi wake. Lifti inatumia sekunde 60 kufika ghorofa ya kumi. Huo ndio muda ulionao. Leo tunaenda kutazamia maelezo yako mafupi.'

**Utendaji**
1. Elezea utatumia njia gani kuangalia maelezo kwa ufupi na kwanini umetumia njia hii.
2. Baada ya kila maelezo, waeleze vijana kuandika jina la mtu ambae wamemtazama na neon moja kuelezea nini wanafikiria kuhusu maelezo hayo kwa ufupi.
3. Baada simulizi 5, tathmini kwa ufupi kulingana na yale vijana waliyoandika.
4. Baada ya masimulizi yote, una tathmini nyingine ya tafakuri ya maelezo ambayo kwayo umetoa mrejesho na kuwaambia umegundua nini na kitu gani waboreshe.

**Tafakuri**
Tafakuri ya mwishoni mwa zoezi hili inakupa mrejesho wa jumla wa yale uliyotazama. Hakikisha mrejesho wa yale wanayosema unakuwa zaidi wa kupongeza, kama ambavyo vijana wanavyojitahidi kusisitiza sifa zao pia. Jitahidi kutoa dondoo za namna ya kuboresha masimulizi yao na namna ya kufanya yawe na maana.

***Dondoo***

Weka tayari kamera ya video (tumia simu yako au simu ya msimuliaji) kwa ajili ya kurekodi masimulizi, ili vijana waweze kuhifadhi maelezo yao mafupi na kuhariri au kuboresha wakihitaji. Hakikisha masimulizi ni ya matumizi ya mtu binafsi tu na hayatatumika nje ya darasa. Fanya tathmini yako kwa kuandika wakati wa masimulizi. Unaona nini? Utapitia maelezo haya wakati wa tafakuri mwishoni mwa kipindi hiki. Linda muda: simulizi idumu kwa sekunde 60 tu. Unaweza kutumia kilinda muda au kengele kwenye simu yako. Sisitiza umuhimu wa kutumia maelezo kwa ufupi kwenye usaili. Au usaili wa kwanza kwa ajili ya mafunzo kazini. Vijana wahifadhi maelezo yao mafupi kwenye simu zao: ili waweze kuboresha kama watahitaji kufanya hivyo. Waambie vijana kwamba wanaweza kukariri masimulizi yao, hivyo wanaweza kurudia au kutumia sehemu yake ili kutengeneza mvuto kwenye hali mpya.

**Uchunguzi wa kina**
Fanya zoezi hili mara nyingi katika mwaka. Hii itawafanya vijana kujiamini kwa kile wanachokimudu, ambacho kitazalisha masimulizi bora sana. Zoezi hili ni muhimu kwa vijana kugundua kama wanapiga hatua.

1.15

# VIPAJI VILIVYOJIFICHA: MWANGAZA WA JUA LA MCHANA!

**Lengo**
Vijana wajizoeshe namna ya kuuliza na kutoa mrejesho kuhusu vipaji vyao vilivyojificha kisha. Watarejea katika vipaji vya wenzao vilivyojificha.

**Maandalizi**
Hakikisha kuna chumba cha kutembea tembea, hakuna meza wala viti. Hakikisha una karatasi (A4) na kalamu za kutosha.

**Maelezo**
'Tabia ya kuwa na kipaji ni kwamba mara nyingi unashindwa kufahamu kitu gani unakiweza zaidi. Hii ni kwa sababu kipaji hiki kinakuja kiasili kwako. Hii ndio tunaita 'kipaji kilichojificha'. Wakati wa zoezi hili, utapata mrejesho kuhusu vipaji vyako vilivyojificha.'

**Utendaji**
1 Bandika kipande cha karatasi (A4) kwenye mgongo wa kila mmoja na hakikisha kila mmoja ana kalamu.
2 Waeleze vijana kutembea kwenye chumba na waulizane 'unaona vipaji vilivyojificha ndani yangu? Tafadhali andika kwenye karatasi'.
3 Kama ndivyo, waambie waandike sifa, uwezo kwa wanafunzi wenzao kwenye karatasi zilipo kwenye migongo yao.
4 Pale watakapomaliza kuandika vitu fulani kwenye mgongo wa mtu, wataendelea na mwingine pia, uliza kama anaona vipaji vilivyojificha na mueleze mtu huyo kuviandika kwenye karatasi.
5 Zoezi hili linaweza kudumu kwa dakika kumi, au kulinga na uwezo wa kikundi, au muda utakapoona kwenye kila karatasi kuna vipaji kadhaa vimeandikwa.
6 Waeleze kushirikiana katika jozi, yale yaliyoandikwa kwenye karatasi migongoni mwao.
7 Waache vijana wachukue picha ya karatasi hiyo, ili waweze kuihifadhi.

**Tafakuri**
Waulize vijana wanajisikiaje kuzunguka namna hii. Wamegundua nini? Wamefikiria nini kuhusu kuandika kitu kwenye mgongo wa mtu mwingine? Wamevutiwa na kile kilichoandi kwa kwenye karatasi zao? Hakikisha vijana hawahukumu sana.

***Dondoo***
Sisitiza umuhimu wa kutoa mrejesho chanya mwanzoni mwa zoezi. Zoezi hili halihusu kutoa mchango hasi wa mawazo. Jiunge na kundi, waulize washiriki wa kueleze vipaji vyako vilivyojificha na andika kitu kwenye karatasi ya kila mwanafunzi. Njia nzuri ya kutoa pongezi isiyotegemewa!

**Uchunguzi wa kina**
Kama unahisi kwamba kundi lina usalama wa kutosha, unaweza kuongeza mazoezi yafuatayo: 'Andika (kwenye karatasi nyingine) kitu ambacho ungependa kujifunza kutoka kwa mwanafunzi huyo'.

# 1.16

# VIPAJI VILIVYOJIFICHA KWENYE KUNDI LETU

KARATASI YA ZOEZI 1.16

**Lengo**
Vijana watafakari kuhusu vipaji vyao wa kutumia yale wenzao waliyosema kuhusu wao.

**Maandalizi**
Hakikisha kuna seti za kutosha za kadi zikiwa na sifa kutoka karatasi ya zoezi 1.16 'Vipaji ndani ya kundi letu'. Utahitaji seti kwa kila washiriki wawili. Weka kadi kwenye bahasha. Unapohitaji seti mpya ya kadi, unaweza kuipakua kutoka www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet. Utakuta viunganishi kwenye programu ya Maendeleo ya Kazi, Mada hii na karatasi hii ya zoezi.

**Maelezo**
'Wakati wa zoezi hili, tutajifunza ni vipaji gani tunadhani kila mmoja wetu anavyo. Tutafanya hivi kwa kutumia kadi nyingi ambazo zina kila aina ya vipaji vilivyochapwa ndani yake. Kisha tutaulizana maswali.'

**Utendaji**
1. Gawa kundi katika jozi na wapatie seti ya kadi za karatasi ya zoezi 1.16 'Vipaji ndani ya kundi letu'.
2. Waache vijana waweke kadi kwenye meza wakizielekeza juu.
3. Kijana mmoja kutoka kila jozi (A) atachagua kadi tano zenye vigezo ambavyo anadhani vinamfaa mtu mwingine (B) naatamu onesha kadi hizo (B).
4. Kijana (A) afafanue kwanini amechagua vigezo hivi kwa mwanakikundi mwenzake (B) na katika hali gani yeye (A) alimuona akitumia vigezo hivi. Je, mhusika (B) anatambua vigezo hivi? Kivipi? Kwa hali zipi? Baada ya hili, muelekeze kijana (B) aandike vipaji hivyo kwenye daftari lake la kumbukumbu na (A) arudishe kadi, akiielekeza juu, kwenye meza.
5. Kisha kijana (B) sasa atachagua kadi 5 ambazo anadhani zitatumika kwake. Mwanafunzi (B) ataonesha kadi hii kwa mwanakikundi (A), Atampatia pongezi zake kwanini amechagua vipaji hivyo na atampa mfano wa nyakati ambazo alitumia vipaji hivyo. Mueleze mshiriki (B) aongeze vipaji vyake kwenye orodha.
6. Rudia zoezi hili. Sasa ni zamu ya (B) kuchagua kadi yenye vipaji ambavyo anadhani vinamfaa mwanakikundi (A). Kwa mara nyingine akiwa na maelezo ya kijana (B) na kijana (A) ataandikavipaji 5 na atamchagulia kadi tano.
7. Hakikisha kuwa wote wanaorodha ya vipaji 10. Waelekeze waweke kadi kwenye bahasha. Bado unazihitaji kwa ajili ya kundi jingine.

**Tafakuri**
Unafikiria nini kuhusu kufanya kazi kwa namna hii? Wamesikia vitu vipya kutoka kwa wanakikundi wenzao, kitu chenye maana fulani kwa mustakabali wao? Wameifurahia vipi orodha ya vipaji?

***Dondoo***

Kwa zoezi hili, ni muhimu kusisitiza kwamba inahusiana na kulenga kipaji cha mtu, sifa zake chanya na uwezo wake. Unaweza kujiongezea kadi nyingi zenye vipaji ambavyo unadhani kwamba havipo na uviongezee kwenye kadi zilizopo. Vijana wanaweza kufanya hivyo hivyo kwa vipaji vilivyokosekana.

**Uchunguzi wa kina**
Namna nyingine ya kufanya zoezi hili ni kutumia kadi kwenye mkutano kundi. Mtu mmoja atachukua kipaji kwenye seti na atampatia kadi hii mwenzake kwenye kundi lenye kipaji hicho. Waache waelezee ni katika hali gani ambayo mtu huyo anaonesha kipaji hicho. Muulize mtu huyo kama anakitambua kipaji hicho. Kisha kadi nyingine itachukuliwa na mtu mwingine na itaelekezwa kwa mtu mwingine. Pale ambapo hakuna mtu mwenye kipaji hicho, chukua kadi nyingine.

# 1.17 MTAZAMO BINAFSI (SELFII)

**Lengo**
Vijana waoneshe wenzao wao ni kina nani kwa kuorodhesha sifa zao na wawape wenzao wasaa wa kuongezea sifa hizo.

**Maandalizi**
Hakikisha vijana wana chumba cha kutosha kubandika maandishi yao kwenye ukuta na washiriki wote waweze kuzunguka kuangalia kazi zao. Hakikisha kuna karatasi kubwa za kutosha, kalamu za wino mzito za rangi tofauti na gundi ya kubandikia.

**Maelezo**
'Tutafanya uchambuzi binafsi wa uwezo wetu. Tuna taswira binafsi, kwa kutambua au kutotambua. Lakini taswira zetu binafsi si muhimu kulingana na namna watu wanavyotuchukulia au wanavyotufuata. Hivyo, katika zoezi hili tutatafiti kama taswira zetu binafsi zinaendana na zile ambazo wengine wanazo kuhusu sisi.'

**Utendaji**
1. Kila mmoja atapata karatasi kubwa na kalamu kadhaa zenye wino mzito.
2. Waeleze vijana waandike majina yao kwenye karatasi kubwa na uwezo wao/sifa zao ambazo wanaweza kuzifikiria. Sifa zote wanazoonesha shuleni/kazini na nyumbani zinaruhusiwa.
3. Waeleze vijana watundike karatasi ukutani.
4. Waeleze vijana wazunguke na watazame taswira binafsi za wenzao. Hakikisha wanapata nafasi ya kufafanua kazi zao na kuuliza maswali. Pia wanaruhusiwa kuongeza sifa kwenye orodha ya wanakikundi wenzao.
5. Waeleze vijana wapige picha taswira zao binafsi.

**Tafakuri**
Waulize vijana wanagundua nini kujaza taswira zao binafsi. Wameona ni rahisi kuelezea uwezo wao? Wamejisikia vipi kuongezea uwezo kwenye orodha za wengine? Wamepata urahisi kufanya hivyo, au hapana? Wamegundua vitu kuhusu wao ambavyo hawakuwa wakijua kabla ya zoezi hili? Je, watu wengine wameongezea uwezo ambao hawakuwahi kutambua kuwa wanao?

***Dondoo***
Shiriki endapo kila mmoja tayari amealikwa kuongeza sifa kwenye orodha ya wanafunzi wengine. Ni nafasi mahsusi ya kutoa pongezi zisizotegemewa.

# 1.18 HOJI KIPAJI CHAKO

**Lengo**
Vijana wachangie mawazo na mrejesho juu ya vipaji vya wanakikundi wenzao na wapewe mrejesho kuhusu vipaji vyao.

**Maandalizi**
Andaa meza katika namna ambayo vijana wataweza kufanya kazi watatu watatu.

**Maelezo**
'Watu wengi kila mara huona kwa uwazi vipaji vyetu ni vipi, lakini hawawezi kutuambia. Mara nyingine huwa tunadhani ni kawaida kuweza kitu fulani na wakati mwingine hatujui namna ya kupongezana. Wakati wa zoezi hili, tutaangazia kipaji cha kila mmoja. Hii ni namna ya kutengeneza mtandao. Unatumia watu wengine kuweza kujua vitu fulani kukuhusu mwenyewe. Kwa upande mwingine kwa kuangazia kwenye vipaji vyao na kwa kuwapongeza wanakikundi wenzao.'

**Utendaji**
1. Ligawe kundi kwa orodha ya watu watatu watatu.
2. Waeleze vijana kuchagua majukumu: A, B na C. Kisha, mtu A atatoa mrejesho kwa B, na C ataandika alichosema A. Watazungumzia mambo yafuatayo katika mzunguko wa kwanza:
   - Ni kitu gani kijana (A) anaona kama kipaji kwa mwanakikundi (B)?
   - Ni jukumu gani kijana (A) angependa kumpangia (B)?
   - Ni kipaji gani ambacho (A) anadhani mwenzake (B) atatumia?
   - Ni kitu gani (A) anadhani (B) anakiweza isivyo kawaida?
   - Fikiria kwamba (B) atahamana (A) - anaetoa mrejesho - atampa neno la kwaheri (B), ni kitu gani (A) atasema kwa (B)?
3. Baada ya mzunguko wa kwanza, badilisha majukumu. Mzungukowa pili (B) atatoa mrejesho kwa (C), (A) ataandika na baada ya hapo mzunguko watatu (C) atatoa mrejesho kwa (A) na (B) ataandika. Wataongelea kitu kile kile, badilisha herufi tu kwenye maelezo.

**Tafakuri**
Waulize vijana wamegundua nini wengine wanapotaja vipaji vyao. Kuna mambo ambayo hawakuwahi kusikia kabla? Wamejisikiaje hasa hasa kupokea mrejesho chanya?

***Dondoo***
Kwa mara nyingine, zoezi hili linahusu kutoa mrejesho chanya. Vijana wanatakiwa kupeana mrejesho chanya, kadri watakavyogundua vipaji vyao kupitia macho ya wanakikundi wenzao.

**Uchunguzi wa kina**
Watie moyo vijana wakawaulize wanafamilia au watu walio karibu nao wajibu maswali hayo hayo na waandike majibu.

# 1.19

# SHAIRI LA KITIBETAN

KARATASI YA ZOEZI 1.19

**Lengo**
Vijana watunge mashairi yao yenye muundo wa shairi la Kitibetan na waelezee fikra zao za ndani na hisia zao.

**Maandalizi**
Hakikisha unajua namna ya kutunga shairi la Kitibetan; tunga shairi moja nyumbani kuona linavyoundwa au toa maelezo kwa rafiki au mwenzako. Panga meza kwa muundo ambao vijana watafanya kazi kwa ukimya na kujitegemea. Unaweza kuweka muziki wa taratibu kwa mbali, wakati vijana wanashughulika na mashairi. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 1.19 'Shairi langu' au andika muundo wake katika ubao.

**Maelezo**
'Kawaida sio rahisi kufafanua hisia zako za ndani. Kwa mfano, unaweza kuwa katika hali ambayo hujisikii huru kuzungumzia hisia zako. Au unaogopa kuchekwa au unadhani watu watakushangaa. Hivyo, ni muhimu kujifunza namna ya kuelezea hisia zako. Kwa sababu hisia zipo siku zote; hakuna namna ya kuzizuia. Kuna aina nne za hisia: hofu, hasira, huzuni, na faraja. Tutafanya kitu na hisia hizi muda wa zoezi hili: tunaenda kuandika shairi la kitibetan. Ni mbinu ya kusafisha kichwa chako na kukuta na hisia zako. Hauhitaji kutunga mistari mizuri, wala haina haja ya kuwa na vina. Kitu cha muhimu ni kuandika kile kinachokuja kwenye mawazo yako kwanza, na kinachopita kichwani kwako muda huu, sasa hivi.'

**Utendaji**
1 Gawa muundo mtupu wa shairi uliopo kwenye karatasi ya zoezi 1.19 'Shairi langu'.
2 Kwanza, waache vijana wawe makini kwa muda kabla hujawaruhusu kufanya zoezi. Hakikisha kundi lipo kimya. Waeleze kwamba kuanzia muda huu (kuanzia muda ambao umepiga muziki kwa mfano) kila mtu lazima akae kimya mpaka shairi litakapoisha.
3 Waambie vijana wachague neno muhimu (kitomeo), dhamira, tendo au kitu kitakachowafanya akili zao kutumika muda huu. Wakumbushe zoezi lao lililopita, ujuzi waliopata, na malengo waliyounda n.k.
4 Anza uandishi wa shairi na wasaidie vijana - mstari kwa mstari - ambacho wanahitaji kuandika.

*Shairi la Kitibetan: maelezo*

| | |
|---|---|
| Mstari wa 1: | mimi.... (tunga sentensi inayoanza na 'mimi' na kwenye sentensi hiyo tumia neno lako kuu) |
| Mstari wa 2: | nipo....(uleze mahali ulipo) |
| Mstari wa 3: | ninaona... |
| Mstari wa 4: | kitu gani kinaendelea? |
| Mstari wa 5: | mstari unafanana na mstari wa 2 |
| Mstari wa 6: | nijibu lenye mhemuko kwa mstari wa 2: inakufanya ujisikie vipi? |
| Mstari wa 7: | mstari wa sawa na ule wa 4 |
| Mstari wa 8: | nijibu lenye mhemuko kwa mstari wa 7 |
| Mstari wa 9: | sawa na mstari wa 6 |
| Mstari wa 10: | nijibu lenye mhemuko kwa mstari wa 2: inakufanya ujisikie vipi? |
| Mstari wa 11: | sawa na mstari wa 8 |
| Mstari wa 12: | inafana na nini? |
| Mstari wa 13: | sawa na mstari wa 10 |
| Mstari wa 14: | inakupa hisia gani? |
| Mstari wa 15: | sawa na mstari wa 12 |
| Mstari wa 16: | ni lipi jibu lako kwa hilo (nini mwitiko wako kwa hilo)? |
| Mstari wa 17: | sawa na mstari wa 14 |
| Mstari wa 18: | sawa na mstari wa 3 |
| Mstari wa 19: | sawa na mstari wa 16 |
| Mstari wa 20: | sawa na mstari wa 1 |

5 Watakapomaliza mistari yote, waambie vijana wasome mashairi na waelekeze watafakari kuhusu mashairi hayo kwa muda.
6 Waelekeze vijana wasome mashairi mmoja baada ya mwingine katika makundi ya watatu au wanne. Kisha wapatie kazi ya kutoa msimamo wao 'kutoka nyoyoni mwao'. Shairi limewafanyia kitu gani?

**Tafakuri**
Chagua baadhi ya wanafunzi ambao watasoma mashairi hayo kwa sauti. Baada ya mashairi kusomwa, pawe na ukimya kwa muda. Usichambue! Acha shairi lijisemee. Kutakuwa na muda wa kuongea kuhusu namna vijana walichojifunza wakati wanaandika mashairi wakati wa tafakuri. Katika makundi makubwa, unaweza kuwaacha vijana wengine wasome mashairi yao katika muda wa mapumziko wakati wa vipindi vyengine.

***Dondoo***

Fafanua hisia nne za msingi kwa vijana: hofu, hasira, huzuni na faraja. Na katika uandishi wa shairi hili, wanaweza kuchagua moja katika hisia hizi au utofauti katika hisia hizi (kama vile hasira, isiyo na matumaini, furaha, wasiwasi, wenye kukatisha tamaa n.k). Vijana wanaweza kuandika hisia zao za msingi kwenye karatasi au ubaoni. Fafanua kwa uwazi kwamba haitakiwi kuwaza kwa sauti, ila wanatakiwa kuandika kimya kimya kinachoingia katika akili zao kwanza. Kitu kingine ambacho unatakiwa kuweka wazi kabisa ni kwamba wanatakiwa kuandika mara nyingi vitu vile vile kama mwanzo; vitu walivyoandika mistari iliyopita. Waambie wasihofie namna shairi litakavyokuwa mwishoni, ila waeleze wamalize mistari yote kwanza bila kuwaza sana. Vijana wanatakiwa kujisikia kama wana muda wa kutosha kuandika mawazo yao. Kwa upande mwingine, hawatakiwi kupoteza muda mrefu katika kila mstari kufikiria vitu vya kuandika. Nafasi ya kuandika inatakiwa kuwa ya kutosha kiusawa.

# 1.20

# NAJIVUNIA......

KARATASI YA ZOEZI 1.20

**Lengo**
Vijana wagundue na kuonesha sifa binafsi na uwezo; watafakari namna ya kufafanua au kuelezea sifa zao.

**Maandalizi**
Andaa eneo katika namna ambayo vijana watafanya kazi katika jozi kwenye meza. Hakikisha una nakala za karatasi ya zoezi 1.20 'Najivunia.....'.

**Maelezo**
'Mara nyingi tunakuwa hatutambui uwezo wetu, tunachukulia kama vile ni kitu cha kawaida. Katika zoezi hili, utarejea katika baadhi ya mafanikio unayojivunia katika maisha yako. Mafanikio hayo yanaweza kuwa kidogo au makubwa, ya kitaaluma au binafsi. Utachunguza mafanikio haya na kugundua ni sifa gani ulitumia wakati huo.'

**Utendaji**
1. Waelekeze vijana kujibu maswali kwa kujitegemea kwenye karatasi ya zoezi 1.20 'Najivunia....'
2. Vijana wahojiane katika jozi, ambapo watachunguza majibu waliyoandika.
    - Acha waelezane (kwa zamu) yale waliyoandika, na kama ni muhimu, waeleze kuambizana kubainisha hali na matendo.
    - Msaili atamsaidia msailiwa kutaja sifa zilizotumika kupata matokeo.
3. Acha vijana waandike hitimisho binafsi na uelewa wao kuhusu zoezi hili. Je, wanahitaji kukumbuka nini kutokana na zoezi hili?

**Tafakuri**
Waulize vijana nini wanafikiria kuhusu zoezi hili. Je, kuna uzoefu mwingine wanadhani ni ni bora kuufikiria? Mwambie kila mmoja kushirikisha hitimisho kuu walilopata kutokana na zoezi hili.

***Dondoo***

Hili ni zoezi jingine ambalo unaweza kutumia kwa vijana kupata mtazamo wa wazi kuhusu sifa zipi ambazo wanatumia kwa hali ipi. Lengo la zoezi hili ni kwa ajili vijana wajifunze kufafanua vipaji wanavyotumia katika hali halisi za maisha, wakijaribu kufikia malengo yao.

# KUPONI YANGU YA PONGEZI



**KUPONI YANGU YA PONGEZI**

**JINA LANGU:**______________________________

Ningependa kupokea pongezi toka kwenu. Asanteni!

**RUDISHA UJUMBE**

Nimepokea pongezi toka kwa:__________________________(jaza jina lako)

Pongezi zangu kwenu ni:

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

Najua kwamba una hizo sifa, kwa sababu:

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

**Tarehe:** **Mafanikio! Kwa furaha kubwa**

# KARATASI YA ZOEZI 1.11



| | |
|---|---|
| **Fafanua kitu ambacho una fahari nacho; kinaweza kuwa hali au kitu ambacho ulikifanya na wengine wakakulipa kwa pongezi.**<br><br>Fafanua hali hii kwa ufupi.<br>Nini kilitokea? Ilikuwa lini?<br>Nani alikuwa pale? Ulifanya nini? | |
| **Sifa gani ambazo zilikufanya utende jinsi ulivyotenda kwa wakati ule. Ilikuwaje ukafanya kazi nzuri kama hiyo?**<br><br>Iliwezekenaje sifa kama hizi kuonekana kwenye tabia yako?<br>Ulifanya nini?<br>Ni jambo gani ulifurahia zaidi? | |
| **Nini kilichokufanya ujisikie fahari?**<br>**Ni maadili gani yanayounganishwa kwako katika hisia hii ya najivunia?** | |

# KARATASI YA ZOEZI 1.13

# NEMBO YANGU!

MADA YA 1.13

JINA: (Sehemu ya juu)

Jinsi nilivyo: (upande wa kushoto)


- Vipaji
- Sifa
- Aina ya mtu

Chora mchoro au kiashirio kwenye sehemu ya chini.

Ninachoweza kufanya: (upande wa kulia)

- Ujuzi

Weka chochote unachotaka kuandika au kuchora kwenye duara hapo kati.



# KARATASI YA ZOEZI 1.16



| | | |
|---|---|---|
| NINAAMINI | MIMI NI MCHANGAMSHAJI | NINAWEZA KUFANYA UCHAGUZI |
| NINA UJUZI | NINAWASAIDIA WENGINE | MIMI NI MZURI |
| NINA MAWAZO MAZURI | NAWEZA KUTOA MSAADA NA FARAJA | NIMEJIPANGA VIZURI |
| NINAAMINIKA | NINA MAWAZO | NINA NGUVU |

| | | |
|---|---|---|
| NINAWEZA KUSIKILIZA | NINA UJUZI | NIPO HURU |
| NINAPENDA MICHEZO | NAWEZA KUTAFUTA UFUMBUZI | NAWEZA KUPANGA |
| NAWEZA KUSHIRIKIANA | NINA NIA YA MAMBO MENGI | NINAWEZA KUSIMAMA MWENYEWE |
| SIKATI TAMAA KWA URAHISI | NINAWEZA KUTENGENEZA MARAFIKI | MIMI NI MBUNIFU |

# KARATASI YA ZOEZI 1.19

# SHAIRI LANGU

MADA YA 1.19

JINA ______________________________

1 ______________________________

2 ______________________________

3 ______________________________

4 ______________________________

5 ______________________________

6 ______________________________

7 ______________________________

8 ______________________________

9 ______________________________

10 ______________________________

11 ______________________________

12 ______________________________

13 ______________________________

14 ______________________________

15 ______________________________

16 ______________________________

17 ______________________________

18 ______________________________

19 ______________________________

20 ______________________________

# KARATASI YA ZOEZI 1.20

**SEHEMU BINAFSI**

1 Eleza utendaji. Hii inaweza kuwa mafanikio, kitu ambacho umefanya vizuri sana, kitu ambacho umekiendeleza, uamuzi uliofanya n.k. Maswali ambayo yatakuwezesha kutoa maelezo yaufafanuzi ni:

- Nini hasa ulichokifanya?
- Kwanini umekifanya?
- Ni hatua gani ulizichukua? Vitendo gani?
- Ulikuwa na jukumu gani katika tukio hili? (Kazi yako ilikuwa ni nini?) Je, ilikuwa ni jitihada yako? Nani mwingine aliyehusika, ulikuwa na jukumu gani kwao?
- Matokeo yalikuwaje kwa kile ulichokifanya / jinsi ulivyofanya?

2 Jiulize swali linalofuata: 'Kwanini ninajivunia sana utendaji huu?'

3 Ni ujuzi gani uliohitaji kufikia utendaji? Ni sifa gani ulizotumia kufikia kile ulichotaka?

4 Kwa njia gani unaweza kutoa ushahidi wa utendaji wako?



# NAJIVUNIA ...

**UTENDAJI**

Maelezo

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

Kwanini unajivunia utendaji huu?

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

# KARATASI YA ZOEZI 1.20

Ujuzi/sifa

Unawezaje kuthibitisha mchango wako kwenye matokeo?



# NAJIVUNIA ...

MADA YA 1.20

**MAHOJIANO KATIKA JOZI**

1. Badilishaneni mlichoandika kwenye karatasi zenu na kama kuna ulazima ulizaneni ili kufafanua utendaji na hali ambayo ilitendeka.
2. Basi msaili anapaswa kumsaidia msailiwa kuzipa majina sifa ambazo zilitumiwa kufikia utendaji.

**HITIMISHO BINAFSI**

Andika chini hitimisho lako na ufahamu ulionufaika nao kutokana na zoezi hili. Nini unachohitaji ukumbuke katika zoezi hili? Ni sifa zipi za binafsi ambazo zoezi hili limekuonesha? Shirikisha hitimisho moja kwenye kundi zima.

Ufahamu, sifa, mambo mengine ninayotaka kuyakumbuka kutokana na zoezi hili: